**Learning by Ear 2009**

**Media & Information**

**Author: Hope Azeda**

**Redaktion: Ludger Schadomsky**

**Kisuaheli Translation:Eric Ponda**

EPISODE 9

| *CHARACTERS* | |
|---|---|
| Announcer: Male/female | |
| "Young Junior" | Male, 15 years old |
| "Sister P." | Female, 16 years old |
| "Charlie" | Male, 18 years old |
| "Ezra": | Male, 22 years old. Brother to "Young Junior". |

**INTRO**

Hujambo msikilizaji na karibu kwa makala ya leo katika mfullizo wa vipindi vyetu vya Leraning By Ear "Noa Bongo jenga maisha yako" Mambo bado hayajatoa mwangaza kwa wanahabari wetu chipukizi! Sister P, Young J na Charlie bado wako katika harakati ya kutafuta fedha za kujaza nakisi ya bajeti kufadhili mradi wao.Mwaliko katika ofisi ya mbunge haukuzaa matunda ingawa mbunge huyo alikubali kuawasaidia kwa masharti ya kutumia stesheni yao kama chombo cha kisiasa. Bila shaka hawakulifurahia jambo hili.Ungana nasi ujue

mambo yatakayojiri na mwelekeo watakaochukua kufanikisha madi huu.

**SCENE 1**

**The Dot.Com FM radio station late morning.**

| |
|---|
| **SFX Traffic noise is heard and there is loud music being played. Sound of CDs being sorted*.*** |

1. Sister P: Young J, hii studio au ni Disco?

**SFX: Music turned down.**

**2.Young J: Haya sister P wataka kuniambia kwamba**

**Tumefanikiwa????**

**3 Sister P.: Ndio sio mzaha,**

**4,Young J: Wacha mas-hara?**

**5,Charlie: Sio utani**

**6,Young J: Nioneshe hebu nioneshe**

| |
|---|
| **SFX : Opening hand bag.** |

7. Sister P; Hii hapa, Young J.

8. Young J: Mungu ni mkubwa. ***Tumpa tumpampatu***,… Ohh Mungu ni mkubwa, Stesheni yetu imepewa leseni.!

Hohohho, sasa tunaweza kusherehekea. ***Tumpa tumpampa tumpa. Rock and roll***!

9. Charlie: Hehehehe, taratibu. Ezra yuko wapi ? Nilifikiri yuko hapa atusaidie katika ujenzi wa stesheni yetu.

10. Young J: Atarudi sasa hivi. Amekwenda kuwaleta mafundi wa mitambo kuuweka hizi mashini.

11. Sister P: Nafikiri sasa tunakila kitu tunachohitaji .Lakini bado tunahitajika kujifunza mambo ya kimsingi jinsi ya kutumia mitambo hii.

12. Young J: Tunapozungumizia suala la wafanyi kazi, pia ni muhimu kufikiria suala la kumuajiri mfanyi kazi wa usafi.

13. Sister P: Huo ni upuuzi mtupu,tufikirieni juu ya kituo chetu cha redio tukifanye kama chumba chetu cha kulala.Nani atawafanyia usafi na kutenga tenga vitu humu? Hatuwezi kupoteza pesa katika mambo kama hayo….

14. Charlie: Sister P, tunapasa kutafautisha baina ya studio na nyumba ya kulala.Tunachohitaji sasa ni kuelekeza fikra na mawazo yetu katika utayarishaji wa vipindi. Hatuwezi kuchanganya mambo na hatupasi kulichukulia mzaha suala hili ya utangazaji.

15. Young J: Au kusoma magazeti ili tuwape wasikilizaji wetu habari moto moto zinazochipuka.

16. Charlie: Au kuosha sakafu na kupanguza madirisha wakati unapopaswa kwenda kufanya mahojiano.

17. Sister P: Hebu tulifikirie jambo hili kwa makini, ni vipi tutaweza kuandaa vipindi bora kwa wasikilizaji wetu bila ya kuwa na wafanyi kazi wa kutosha?.

18. Young J: Kwanza tunachopaswa kufanya ni kujisajili na magazeti yote ndipo tutaweza kuyatumie kama vyanzo vya habari.

19. Charlie: (**Laughs)** Sister P, Huyu anazungumza kama mtu anayetoka sayari ya Mars.

20. Sister P: Unamaanisha nini, Charlie?

21. Charlie : Si unafahamu kwamba magazeti haya hayachapishwi mara kwa mara.Mengine yanachapishwa baada ya mwezi au mara mbili kwa mwaka.

22. Young J: Wacha hiyo,Na wakati yanapotufikia je , habari hizo huwa tayari zimepitwa na wakati.

23. Charlie: Magazeti yanayochapishwa mara kwa mara ni yale yanayosimamiwa na serikali nayo huwa yanaegemea upande mmoja tu.. upande wa

serikali, ili kuwafahamisha watu kile serikali inachotaka wajue .

24. Sister P: Kwa hivyo tufanyeje, kwani ni lazima wasikilizaji wetu wapashwe habari kadri zinavyochipuka.?

25. Young J: Nakuelewa !

26. Charlie: Endelea.

27. Young J: Tuunganishwe na mtandao wa Intaneti. Ndio njia pekee ya kupata habari moto moto kuwapasha wasikilizaji wetu.

28. Charlie: Mashirika mengi ya habari katika mtandao wa Intaneti huwa na habari moto moto kutoka pembe zote za ulimengu.

**SCENE TWO**

**The balcony outside the Dot.Com FM radio station.**

**SFX Sounds of hammering on walls etc from inside.**

29. Young J: Ezra, unawaamini hao jamaa uliowaleta,hao mafundi

30. Ezra: Ndio kwanini?

31. Young J: Nasikia wakuvunja hizo skru.

32. Ezra: Usijali . Wanaelewa wanchofanya. Na mambo yakienda sawa, huenda tukaanza kupeperusha matangazo hivi leo jioni.

33. Sister P: Wacha mzaha! (**Excited)** Siwezi kusubiri kwani tayari nimeanza kushikwa na mchecheto.

34. Ezra: Usiwe na wasi wasi mambo yataenda vizuri tu!

35. Charlie: Ezra, Kabla ya wewe kufika, tulikuwa tukizungumzia suala la vipindi na jinsi tutakavyoweza kupata habari moto moto kwa wasikilizaji wetu.

36. Ezra: Hilo si tatizo. Mnachohitaji ni kuunganishwa na mtandao wa Intaneti.Kisha kushirikiana na mshirika ya habari ya kigeni ili kupata habari mnazotaka kwa wasikilizaji wenu.Lakini mkitegemea mashirika ya humu nchini mtakuwa mukitatangaza historia.

37 Sister P: Lakini Ezra, mashirika ya kigeni yametawala sana sekta ya habari. Nini kinachoyafanya kuwa hivyo?

38 . Ezra: Kuna sababu nyingi tu, lakini kimsingi ni kwamba mashirika haya yanawaandishi wa habari katika kila pembe ya ulimwengu, sio kama magazeti ya humu nchini..

39. Charlie: Wanawaandishi wa habari katika mataifa yote ulimwenguni.

40. Ezra: Si hayo tu, pia yanasifa ya kuzingatia na kudumisha maadili ya uandishi wa habari hali inayoyafanya kuwa ya kutegemewa na wasikilizaji na wasomaji kote ulimwenguni kwa habari za kuaminika.

41. Sister P: (Interrupting.Excited)Ezra umagonga ndipo.Mara nyingine utakuta jambo linatendeka hapa lakini likapuuzwa na vyombo vya habari vya humu nchini na kulisikia tu katika vyombo vya habari vya kigeni.

42. Ezra: Mashirika hayo ya habari yanavifaa bora vya kukusanya habari. Hebu wangalia wenzako kama bado wanang'ang'ana kuunganisha mtandao wa Nitaneti. Na hata bado hamujaweka laini ya simu. Itakuwa vigumu kufanya kazi katika mazingira haya.

43. Young J: Sasa tufanye nini?

44. Ezra: Tubadilishe hali hii rafiki zangu .Nadhani wakati umewadia kubadilisha hali ya mambo.

45. Sister P: Nini Ezra? Mimi nimejitolea kwa uwezo wangu wote kubadilisha hali hii.

46. Ezra: Kwanini tusianzishe shirika la habari la Africa

47. Charlie: Africa… vipi?

48. Ezra: Yaani shirika la Kiafrica litakalo ripoti habari za Africa na maendeleo ya bara hili la Africa.

49. Sister P: Napenda jinsi Ezra anavyolielezea suala hili…., Shirika la habari la Africa, kuripoti habari za Africa kuhusu maendeleo ya Africa.…lakini sio habari kuhusu magonjwa au migogoro.

50. Charlie: Yote yanaweza kujumuishwa!.

51. Young J: Nadhani hilo ni wazo zuri Ezra.

52. Sister P: Ni utani tu. Kazi bila utani humfanya J. kuwa mnyonge. Lakini naunga mkono wazo hilo.

53. Ezra: Nina orodha ya majina ya waandishi wa habari kutoka mataifa mbali mbali barani Africa.Tukikubaliana naweza kuwasiliana nao ili tuanzisha mtandao wetu wa habari.

54. Charlie: Halafu,tutaweza kupata habari kutoka maeneo yote kaskazini,kusini na mashariki na pia magharibi mwa Africa.

55. Sister P: Na hilo litatusaidia kuepukana na dhiki ya kutafuta habari kuhusu bara hili kutoka kwa mashirika ya habari ya kigeni

56. Joung J: Je tunaweza kukabiliana na ushindani?

57.Ezra : Kwanini tusiweze? Ni kujitolea tu na kuwa na mwelekeo.

58. Charlie: Naamini hata yale mashirika ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu pia yatakuwa na hamu ya kushirikana nasi.

59. Ezra: Tukiwa na shirika kama hili ni rahisi kuwapa wasikilizaji wetu habari moto moto wakati wote.

60. Sister P: Tukubaliane kisha tuanze mikakati ya kuanzisha shirika hili na bila shaka tutafanikiwa.Tuliiteje?

61. Young J: ***"Africa News".***

62. Charlie: Ni kama jina la shirika la kigeni.

63. Ezra: Maoni yako Charlie?

64. Charlie: Bado nafikiria .

65. Sister P: Au tuliite PANA?

66. Ezra: Panya kwa lugha ya Swahili ni mnyama.Tutawezaje kutumia jina hilo kwa shirika letu Sister P.

67. Sister P: Sijasema Panya. Nimesema PANA…The Pan African News Agency. Nadhani hilo ni jina zuri, mwasemaje?

End

**OUTRO**

Basi umeyasikia , waandishi wetu wahabari bado wamo mbioni, hawajatosheka na kituo cha redio na sasa wanataka kupanua

shughuli zao na kuanzisha shirika kubwa la habari litakalo tegemewa kwa habari za Africa kutoka barani Africa.Je Upo? Kwa maoni yako unadhani mashirika ya habari ya kigeni yanaandika habari zisizo sahihi kuhusu bara la Africa? Tuma maoni yako kuhusu suala hili au jambo lolote linalokukera kwa kundi letu la Learning by Ear hapa mjini Bonn. Unaweza kufanya hivyo kwa kutumia mtandao wetu wa dw-world.d e/lbe.

Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.!